**ISSN 1866-5866** JULAI - SEPTEMBA, **2025**

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
TANZANIA COMMISSION FOR HUMAN RIGHTS AND GOOD GOVERNANCE

THE VOICE OF
# Haki
JARIDA LA TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

# THBUB YATOA WITO KWA ASKARI POLISI KUSIMAMIA HAKI



*Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mhe. Mathew P. M. Mwaimu (Jaji Mst) (wa tatu kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa wa Jeshi la Polisi na Viongozi wao mara baada ya kufungua mafunzo kuhusu haki za binadamu na wajibu wa Jeshi la Polisi wakati wa Uchaguzi Mkuu 2025, yaliyofanyika Jijini Dodoma Septemba 16, 2025.*

**NDANI** **THBUB YAFUNGUA TAWI TABORA**

# NENO LA **UTANGULIZI**

**Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ni idara huru ya Serikali, iliyoanzishwa kama Taasisi ya kitaifa iliyo kitovu cha kukuza na kulinda Haki za Binadamu na misingi ya Utawala Bora nchini Tanzania.**

**THBUB ilianzishwa chini ya Ibara ya 129(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 3 ya mwaka 2000.**

**THBUB imepewa jukumu la kupokea na kuchunguza malalamiko ya uvunjifu wa haki za binadamu, kufanya ufafiti, ufuatiliaji wa masuala ya haki za binadamu na utawala bora sambamba na kutoa elimu.**



**Mhe. Mathew P. M. Mwaimu (Jaji Mst)**
Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

**Uanzishwaji wa jarida la Voice of Haki umelenga kutoa taarifa ya kazi mbalimbali zinazofanywa na THBUB ili kuweka uelewa kwa jamii kuhusu majukumu ya Tume na namna majukumu hayo yanavyotekelezwa katika kulinda na kukuza haki za binadamu na misingi ya utawala bora.**

**Hivyo, nichukue fursa hii kuwakaribisha kusoma jarida la robo ya kwanza kwa mwaka 2025/2026 ili kuweza kuifahamu THBUB pamoja na majukumu yake.**

**KAMATI YA UHARIRI**
**Mwenyekiti:**
Monica Mnanka
**Mhariri:**
Zawadi A. Msalla
**Mhariri Msaidizi:**
Nuru Mfaume
**Wajumbe:**
Mwashamba Juma
Tumaini Obel
Farida Ruben

**MAWASILIANO**
Mtaa wa Nyerere,
Plot Na. 339/Kilimani
S.L.P 1049 DODOMA,
Tanzania
Simu: +255 738 279744
Barua Pepe:
www.chragg.go.tz

## YALIYOMO


| | |
|---|---|
| THBUB YATOA WITO KWA ASKARI POLISI KUSIMAMIA HAKI | UK. 3 |
| THBUB YAFUNGUA TAWI TABORA | UK. 4 |
| WIZARA YA KILIMO KUSHIRIKIANA NA THBUB KATIKA ULINZI WA HAKI ZA WAKULIMA NA WAFUGAJI. | UK. 5 |
| THBUB YAIASA JAMII KUWATUNZA NA KUWATHAMINI WAZEE | UK. 6 |
| WAANDISHI WA HABARI WATAKIWA KUZINGATIA MAADILI YA TAALUMA YAO KULINDA HAKI ZA BINADAMU. | UK. 7 |
| THBUB YAFIKISHA HUDUMA KWA WANANCHI MAONESHO YA SABASABA | UK. 8 |
| WANAMICHEZO THBUB WASHIRIKI MASHINDANO YA SHIMIWI JIJINI MWANZA | UK. 9 |
| HABARI PICHA | UK. 10 |
| HABARI PICHA | UK. 12 |
| HABARI PICHA | UK. 13 |

# THBUB YATOA WITO KWA ASKARI POLISI KUSIMAMIA HAKI

**Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB),** imetoa wito kwa Jeshi la Polisi kusimamia haki wakati wa utekelezaji wa majukumu yao kabla, wakati na baada ya uchaguzi ili wananchi waweze kupata fursa ya kutimiza haki yao ya kikatiba ya kuchagua viongozi wao.

Wito huo umetolewa Septemba 16, 2025 Jijini Dodoma na Mwenyekiti wa Tume hiyo, Mhe. Jaji (Mst) Mathew P. M. Mwaimu wakati akifungua mafunzo ya siku moja kwa maafisa 827 wa Jeshi la Polisi kuhusu haki na wajibu wao wakati wa Uchaguzi Mkuu 2025. Mafunzo kwa maafisa wa Jeshi la Polisi yamefanyika katika mikoa 19 ya Tanzania Bara na Zanzibar kati ya tarehe 16 na 20 Septemba, 2025.

Mhe. Jaji (Mst) Mwaimu amesema Jeshi la Polisi lina wajibu wa kujiepusha na migogoro isiyo ya lazima wakati wa uchaguzi, badala yake kuhakikisha usalama wa watu na mali zao katika kipindi chote cha uchaguzi. Kwa kufanya hivyo, haki za binadamu zitaheshimiwa na kulindwa kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

Akizungumzia majukumu ya THBUB, Mhe. Jaji (Mst) Mwaimu amesema Tume hiyo inalo jukumu la kuhamasisha hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na utawala bora. Jukumu ambalo limeainishwa katika Ibara ya 130(1)(a) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 6(1)(a) na (d) cha sheria ya THBUB, Sura ya 391.

Naye mwakilishi wa Mkuu wa Polisi Wilaya ya Dodoma Mjini , Bi.Grace Salia ambaye ni Mratibu Mwandamizi wa Polisi amesema mafunzo yaliyotolewa kwa maafisa hao yatawasaidia kufanya kazi kwa weledi na kwa kuzingatia haki za binadamu.

"Tutazingatia sheria, taratibu na kanuni pamoja na kulinda haki za binadamu ukizingatia kuwa nchi yetu imesaini mikataba mbalimbali ya kimataifa inayohusiana na ulinzi wa haki za binadamu, "amesisitiza Bi. Salia.




*Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mhe. Mathew P. M. Mwaimu(Jaji Mst) akitoa hotuba ya ufunguzi wa mafunzo kuhusu haki za binadamu na uzingatiwaji wa misingi ya utawala bora katika mchakato wa uchaguzi,kwa Maafisa wa Jeshi la Polisi yaliyofanyika katika Ukumbi wa Askari Septemba 16,2025 Jijini Dodoma*

# THBUB YAFUNGUA TAWI TABORA

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora(THBUB) imefungua ofisi ya Tawi katika Mkoa wa Tabora Julai Mosi 2025 itakayohudumia mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi ikiwa ni jitihadaza kufikisha huduma zake kwa maeneo mengine ya nchi ili kuwafikia watu wote.

Akieleza kuhusu ufunguzi wa ofisi mpya ya THBUB, Katibu Mtendaji wa THBUB, Bw. Patience Ntwina, amesema lengo la kufunguliwa kwa ofisi hiyo mkoani hapo ni kuendelea kutanua wigo wa utoaji wa huduma za THBUB kuwafikia watu wengi zaidi wanaofika kuwasilisha malalamiko yao ya uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Kupata elimu na ushauri wa kisheria kuhusu Haki za Binadamu.

Aidha, Bw. Ntwina ameeleza kuwa awali malalamiko ya wakazi wa Mkoa wa Tabora na mikoa jirani yalishughulikiwa katika Ofisi za THBUB Makao Makuu Dodoma jambo ambalo lilisababisha baadhi ya malalamiko kutoshughulikiwa kwa wakati. Hali ambayo imeleta usumbufu na uhitaji wa THBUB wa kuwa na ofisi mkoa wa Tabora.

THBUB imejipanga kuyafikia makundi mengi zaidi katika mkoa wa Tabora na mikoa ya jirani kwa njia ya kutoa elimu ya haki za binadamu na utawala bora kupitia klabu za shule za sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu, vipindi ya redio, mikutano ya hadhara na mafunzo.

## TUNAPATA MAFUNZO



*Askari wa Jeshi la Polisi na Waandishi wa Habari wakipatiwa mafunzo na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kuhusu haki za binadamu na wajibu wao wakati wa uchaguzi mkuu yaliyofanyika Septemba, 2025 katika Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza.*




*Mkurugenzi Msaidizi Elimu kwa Umma na Mawasiliano Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Bi. Zawadi Msalla akieleza majukumu ya THBUB kwa Naibu Katibu Mkuu Wizara Kilimo Mhandisi Athuman Kilundunya wakati alipotembelea banda la THBUB katika Maonesho ya Nanenane Jijini Dodoma Agosti 4,2025.*

# Wizara ya Kilimo kushirikiana na THBUB katika ulinzi wa haki za wakulima na wafugaji

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Mhandisi Athuman Kilundunya amesema kuwa Wizara ya Kilimo ipo tayari kushirikiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika ulinzi wa haki za binadamu kwa jamii ya wakulima na wafugaji ili kupunguza migogoro kati ya jamii hizi.

Mhandisi Kilundunya ameyasema hayo Agosti 4,2025 wakati alipotembelea banda la THBUB katika Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika Viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma kuanzia tarehe 01-08 Agosti, 2025.
Akielezea madhara ya migogoro ya wakulima na wafugaji, Mhandisi Kilundunya ameeleza kuwa migogoro iliyopo kwa baadhi ya maeneo ya Wafugaji na Wakulima imesababisha kuvunjwa kwa haki za binadamu ikiwemo haki ya kuishi.

"Tushirikiane katika kutatua migogoro, THBUB mnaweza kutuletea ushauri kutokana na chunguzi mnazozifanya zinazohusu masuala ya wakulima na wafugaji tusaidie ndugu zetu" amesema Mhandisi Kilundunya.

Awali, wakati akielezea majukumu ya THBUB, Mkurugenzi Msaidizi Elimu kwa Umma na Mawasiliano, Bi.Zawadi Msalla amesema Wizara ya Kilimo ni kati ya wadau muhimu wa THBUB na ameahidi kuendeleza ushirikiano na wizara hiyo. Aidha, Bi. Zawadi amesema kuwa, THBUB imeshiriki katika maonesho ya Nanenane 2025 katika mikoa ya Dodoma, Morogoro na Mwanza ili kutoa elimu ya haki za binadamu, ushauri wa kisheria pamoja na kupokea malalamiko ya uvunjifu wa haki za binadamu na utawala bora.

Katika maadhimisho hayo, jumla ya wananchi wapatao 12,364 walitembelea mabanda ya THBUB na Machapisho 2,779 yaliyohusu Utaratibu wa Kuwasilisha na kufuatilia Malalamiko THBUB na Utawala Bora (Dhana, Maana na Umuhimu) yaligawiwa.




*Kamishna Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Mhe. Khatibu Mwinyi Mwinyichande akikabidhi mahitaji muhimu kwa Wazee waishio kituo cha Welezo kilichopo Wilaya Magharibi A, Mkoa wa Mjini Magharibi Oktoba 11,2025.*

# THBUB yaiasa jamii kuwatunza na kuwathamini wazee

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeishauri jamii kuwatunza, kuwathamini na kuwaenzi wazee kwa kuwa ni sehemu ya jamii.

Kauli hiyo imetolewa na Kamishna wa THBUB Ofisi ya Zanzibar, Mhe. Khatibu Mwinyi Mwinyichande alipotembelea vituo vya kulea wazee vya Welezo na Sebleni wakati wa kilele cha kuadhimisha Siku ya wazee duniani ambayo hufanyika Oktoba 01 ya kila mwaka.

Mhe. Mwinyichande amesema wazee wana thamani na umuhimu kutokana na wao kuwa ndio chimbuko la kuwepo kwa mafanikio yaliyopatikana katika nchi hii .
"Sote ni mashahidi wa hilo, tunaona majengo mazuri yaliopo, huduma za afya, viongozi mahiri, waliopita na waliopo sasa hivi pamoja na amani iliyopo nchini, yote hayo yanatokana na wazee wetu hawa," alisema.
Kamishna Mwinyichande ametumia fursa hiyo kuwakumbusha wazee kutumia haki yao ya kikatiba ya kushiriki kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025.

Aidha, Mkuu wa Kituo cha Kulelea Wazee hao cha Welezo, Mkoa wa Mjini Magharibi, Khamis Ali Haji amesema wazee hao wako tayari kupiga kura kwa kuwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) imeshaandaa mazingira mazuri ya kuwawezesha kupiga kura katika eneo hilo na kwamba wazee wa kituo hicho wanapata malezi mazuri kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee na kupata haki zote wanazostahiki. Naye Kaimu Mkuu wa Kituo cha Kulea Watoto Sebleni, Harusi Sadik Rashid akizungumza mara baada ya kukabidhiwa zawadi na Kamishna Mwinyichande, alitoa shukurani kwa THBUB kwa kuona umuhimu wa kuwatembelea wazee hao na kuwapatia zawadi za vyakula, maji safi, dawa na vifaa mbalimbali vya usafi pamoja na kufanya usafi eneo la makazi ya wazee.

Katika maadhimisho hayo ya siku ya wazee duniani, viongozi na watumishi wa THBUB walifanya usafi katika eneo la makazi ya wazee na kuwakabidhi msaada wa vifaa mbalimbali ikiweo mchele, sukari, sabuni dawa pamoja na vifaa vya usafi.

# Waandishi wa habari watakiwa kuzingatia maadili ya taaluma yao kulinda Haki za Binadamu



***Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) , Mhe. Mohamed Khamis Hamad akifungua mafunzo kwa waandishiwa habari kuhusu haki na wajibu wao wakati wa Uchaguzi Mkuu 2025 yaliyofanyika katika Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Jijini Arusha Septemba 17,2025.***

Vyombo vya habari vina nafasi muhimu katika kuhakikisha jamii inapokea taarifa sahihi na zenye kuelimisha. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) kwa kutambua mchango wa vyombo vya habari wakati wa uchaguzi, imetoa wito kwa waandishi wa habari nchini kuzingatia maadili ya taaluma yao katika kuhabarisha Umma katika kipindi kabla, wakati na baada ya uchaguzi Mkuu Octoba 2025 ili kulinda haki za binadamu.

Wito huo umetolewa na Makamishna, Wakurugenzi na watumishi wa THBUB wakati wakifungua mafunzo ya siku moja ya waandishi wa habari yaliyolenga kuwajengea uwezo waandishi hao kuhusu haki za binadamu na wajibu wa waandishi wa habari wakati wa uchaguzi yaliyotolewa katika mikoa 19 ya Tanzania Bara na Zanzibar kati ya tarehe15 na 20 Septemba, 2025.

Akifungua mafunzo yaliyofanyika katika katika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Jijini Arusha Septemba 17, 2025, Makamu Mwenyekiti THBUB, Mhe. Mohamed Khamis Hamad amewakumbusha waandishi wa habari kuwa wana wajibu wa kuripoti habari zao kwa usahihi, kwa uwiano na bila upendeleo kwa chama au mgombea yeyote. Aidha, amewataka waandishi wa habari kuepuka matumizi ya lugha ya matusi, kejeli, udhalilishaji, pamoja na kuchapisha au kutangaza taarifa zenye viashiria vya uchochezi, hasa kupitia mitandao ya kijamii.

"Vyombo vya habari ni kiungo muhimu kati ya wananchi, wagombea na taasisi za uchaguzi, hivyo vinapaswa kuwa chanzo cha taarifa sahihi na si chombo cha kueneza taarifa za uongo na potofu. Maadili ya uandishi, uhuru wa habari na ulinzi wa haki za binadamu ni nguzo muhimu zinazopaswa kupewa kipaumbele "amesisitiza Mhe. Mohmed



*Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Mhe. Nyanda Shuli akitoa elimu ya haki za mtoto kwa baadhi ya Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Wailes iliyoko Temeke Jijini Dar es salaam waliembelea Banda ta THBUB wakati wa Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Sabasaba yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere Jijini humo Julai 11, 2025.*

# THBUB YAFIKISHA HUDUMA KWA WANANCHI MAONESHO YA SABASABA

Zaidi ya wananchi 400 wametembelea banda la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) na kupatiwa elimu ya haki za binadamu na ushauri wa kisheria wakati wa Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba 2025) yaliyofanyika katika Viwanja vya Sabasaba Jinini Dar s Salaam kuanzia Juni 28 hadi Julai 13, 2025.

Huduma zingine zilizotolewa na THBUB wakati wa maonesho hayo ni pamoja na kupokea na kushughulikia malalamiko ya uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Taarifa hiyo imetolewa na Kamishna wa THBUB, Mhe. Nyanda Shuli, alipokuwa akitoa taarifa kwa umma kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Tume hiyo katika kipindi cha maonesho ya Sabasaba Julai 11, 2025.

Kamishna Shuli amesema kuwa wananchi waliotembelea banda la THBUB ni wanawake 195, wanaume 155 na wanafunzi kutoka shule za msingi na sekondari zilizopo Manispaa ya Temeke Jijini Dar es salaam.

Akitoa taarifa ya malalamiko, Kamishna Shuli amebainisha kuwa, THBUB imepokea malalamiko 23 na tayari imeanza kuyashughulikia malalamiko husika. Malalmiko yaliyopokelewa yanahusu migogoro ya ardhi, mafao ya wastaafu, mirathi, na ukatili dhidi ya watoto. Kwa upande wao, wananchi waliotembelea banda hilo wametoa pongezi kwa juhudi zinazochukuliwa na THBUB kusogeza huduma karibu na jamii. "Sikujua kama unaweza kupeleka malalamiko bila kulipa chochote, kiufupi huduma hizi zimetusaidia sana kwani watu wengi wanapoteza haki zao kwa kutojua. Kama Tume itaendelea kusogeza huduma hizi karibu nasi, basi tutapiga hatua kubwa kama taifa." alisema Bi. Rehema Hassan, mkazi wa Temeke.

Kupitia ushiriki wa maonesho, THBUB imeendelea kusogeza huduma zake karibu zaidi na wananchi wa maeneo husika, ikiimarisha uelewa kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

# Wanamichezo THBUB washiriki mashindano ya Shimiwi jijini Mwanza



***Timu ya Kamba Wanaume Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora wakivutana na Timu ya Wanaume Kamba Ikulu katika Mashindano ya Shirikisho la Michezo la Idara za Serikali Septmba 8,2025 Viwanja vya Furahisha Jijini Mwanza***

Watumishi Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora wameungana na watumishi wengine kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kushiriki Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) yaliyofanyika Jijini Mwanza kuanzia Septemba 01 hadi 16, 2025.

Mashindano hayo yaliyobeba kauli mbiu isemayo "Michezo kwa Watumishi Huongeza Tija Kazini:Jitokeze kushiriki Uchaguzi Mkuu 2025 kwa Amani na Utulivu" yamelenga katika kuimirisha afya za watumishi na kujenga ushirikiano baina ya watumishi.

THBUB imeshiriki katika michezo ya kamba ( wanaume na wanawake) ambapo wanaume walifika hatua ya makundi, riadha na karata.

Akizungumza wakati wa michuano hiyo, Kapteni wa Timu ya Kamba wanaume Bw.Kilua Mtae alieleza kuwa timu hiyo ilijipanga ipasavyo katika kuhakikisha ushindi unapatikana. Hata hivyo, Timu ya kamba wanaume ilifanikiwa kushika nafasi ya kumi na sita bora na timu ya kamba wanawake kushika nafasi ya kumi bora.

# HABARI **PICHA**

## **Maonesho Sabasaba** 2025




***Mwandishi Mkuu wa Sheria Bw. Onorious Njole akipatiwa maelezo kuhusu shughuli na majukumu yanayotekelezwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu kwa Umma na Mawasiliano Bi. Zawadi Msalla wakati wa Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Sabasaba yaliyofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere Jijini Dar es salaam Julai 6,2025***

## **Maonesho Nanenane** 2025



***Kamishna wa Maadili Mhe. Jaji (Stahiki) Sivangilwa Mwangesi akizungumza na Watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Bw. Fadhili Muganyizi na Bw. Halfan Botea mara baada ya kusaini kitabu cha wageni alipotembelea banda la THBUB wakati wa Maonesho ya Nanenane Viwanja vya Nzuguni ,Jijini Dodoma Agosti 6,2025.***

## **Maonesho Nanenane** 2025



*Afisa Uchunguzi Mkuu THBUB, Bw.Fadhili Muganyizi akitoa elimu ya Haki za Binadamu na Utawala bora kwa wanafunzi wa chuo cha Mipango walipotembea banda la THBUB wakati wa Maonesho ya Nanenane Viwanja vya Nzuguni Agosti 2, 2025.*

## **Mafunzo Jeshi la Polisi** 2025



*Afisa Uchunguzi Mkuu, THBUB, Bw.Chrisantus Ndibaiukao akitoa mafunzo kuhusu haki na wajibu wakati wa Uchaguzi Mkuu 2025 kwa Maafisa wa Jeshi la Polisi yaliyofanyika katika Ukumbi wa Bwalo la Askari Jinini Dodoma Septemba 16, 2025.*

## **Mafunzo Jeshi la Polisi** 2025



***Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Bw. Patience Ntwina (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa wa Jeshi la Polisi kutoka katika Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni na Watumishi kutoka THBUB mara baada ya kumalizika kwa mafunzo kuhusu haki na wajibu wa Askari wa Jeshi la Polisi katika uchaguzi mkuu yaliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Kituo cha polisi Osterbay Jijini Dar es Salaam, Septemba 19,2025.***




***Kamishna Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mhe. Dkt.Thomas Masanja (wa pili kushoto waliokaa) na maafisa wengine wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora wakiwa katika picha ya pamoja na Askari wa Jeshi la Polisi mara baada ya mafunzo kuhusu haki na wajibu wa Askari wa Jeshi la Polisi katika Uchaguzi Mkuu yaliyofanyika katika yaliyofanyika Mkoani Mara Septemba 19,2025***

## **Mafunzo** Jeshi la Polisi




***Mkurugenzi Idara ya Elimu kwa Umma, Mawasiliano, Utafiti na Nyaraka Bi. Monica Mnanka na watumishi wa THBUB wakiwa katika picha ya pamoja na Askari wa Jeshi la Polisi mara baada ya mafunzo kuhusu Haki na Wajibu wa Askari Polisi wakati wa uchaguzi. Jiji la Tanga Septemba 20, 2025***

## **Maonesho** Jumuiya ya Waislamu




***Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Mhe. Mathew P. M. Mwaimu (Jaji mst) alipotembelea baadhi ya mabanda yaliyoshiriki katika maonesho yaliyoandaliwa na Jumuiya ya Waislam Ah¬madiyya Jinini Dar es Salaam Septemba 27, 2025.***

## **Mkutano** Sekta ya Uvuvi



***Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Mhe. Nyanda Shuli akizungumza wakati akifunga mkutano maalum wa sekta ya uvuvi ulioandaliwa na Tume hiyo kwa kushirikiana na Taasisi ya Haki za Binadamu ya Denmark uliofanyika katika hoteli ya Four Points Jijini Dar es salaam, Julai 17, 2025.***

## **Mkutano**



***Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Mhe. Mohamed Khamis Ham¬ad (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi kutoka THBUB pamoja na Wadau kutoka makampuni ya sekta ya uzalishaji, kilimo, usafirishaji na taasisi simamizi za biashara mara baada ya kumalizika kwa mkutano wa wadau kuhusu uhakiki wa Haki za Binadamu uliofanyika mjini Morogoro Agosti 20, 2025.***

## **Usafi** nyumba ya wazee



*Watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ofisi ya Zanzibar, wakifanya usafi katika nyumba ya kuwatunza wazee, Welezo Wilaya ya Magharibi A, Mkoa wa Mjini Magharibi, 11 Oktoba, 2025 ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya siku ya Wazee Duniani, ambayo huadhimishwa kila mwaka.*

## MICHEZO



*Timu ya kamba Wanawake ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora wakivutana Kamba na Timu ya Wanawake ya Wizara ya Ardhi wakati wa mashindano ya SHIMIWI yaliyofanyika katika viwanja vya Furahisha Jijini Mwanza Septemba3, 2025.*

**MAWASILIANO**

**Mtaa wa Nyerere,** Plot Na. 339/Kilimani

S.L.P 1049 DODOMA, Tanzania

Simu: +255 738 279744

Barua Pepe:

**www.chragg.go.tz**